# STD 6 END TERM 2 EXAM 2019

# KISWAHILI

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 - 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi.***

Hapo __1__ za kale __2__ mtumwa mmoja __3__ alidhulumiwa sana na tajiri __4__, Licha ya kufanyishwa kazi za __5__ kutwa __6__, alicharazwa __7__ mijeledi. Mtumwa __8__ hakuweza kustahimili tena mateso haya. __9__, akaamua kutorokea __10__ kule, na liwe __11__. "Nitaacha kasri __12__ la mfalme na kutafuta usalama. Hapo nitakuwa huru na jitu hili __13__ halitaniona tena."

Kote alijua kwamba alihitaji ujasiri na uangalifu __14__. Bila ya hayo, mpango wake, ungetumbukia __15__. Basi siku moja alingojea mpaka giza totoro lilipokumbatia usiku.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. shamani | B. samani | C. zamani | D. kitambo |
| **2.** | A. kuliishi | B. kuliisha | C. mliishii | D. paliishi |
| **3.** | A. ambalo | B. ambaye | C. ambazo | D. ambayo |
| **4.** | A. yake | B. wake | C. lake | D. zake |
| **5.** | A. kasiraji | B. junguu jiko | C. sulubu | D. kirimiti |
| **6.** | A. kutua | B. kuju | C. kucha | D. kwote |
| **7.** | A. na | B. kati | C. kwa | D. kuwa |
| **8.** | A. hio | B. huo | C. hilo | D. huyo |
| **9.** | A. Tia moyo | B. Alipiga moyo | C. Alipiga moyo konde | D. Alighairi |
| **10.** | A. popote | B. kokote | C. momote | D. pote |
| **11.** | A. lipo | B. lije | C. liwalo | D. liko |
| **12.** | A. hii | B. hili | C. huo | D. hizi |
| **13.** | A. mkarinu | B. mtiifu | C. baili | D. katili |
| **14.** | A. jingi | B. nyingi | C. zingi | D. mwingi |
| **15.** | A. nyongo | B. damu | C. maji | D. usaa |

***Kutoka swali la 16 - 30, jibu swali kulingana na maagizo.***

16. ***Kamilisha tashbihi;***
Kutengana kama ______________
A. mbingu na ardhi
B. shilingi kwa ya pili
C. Mafiga na sufuria
D. Pacha

17. Neno **"maji"** liko katika ngeli gani?
A. U - U
B. U - I
C. YA - YA
D. I - ZA

18. Samaki wengi huitwa ___________
A. kikosi
B. numbi
C. thurea
D. halaiki

19. Dada wa mama huitwa
A. halati
B. mama
C. shangazi
D. dada

20. Mtu anayetengeneza vitu kutokana na vyuma huitwa
A. mhunzi
B. mfinyanzi
C. sonara
D. mkalimani

21. Kamilisha;
Nguo ________ ni chafu.
A. lenyewe
B. yenyewe
C. penyewe
D. yenye

22. Bingu ni rangi ipi?
A. Nyekundu
B. Nyeusi
C. Samawati
D. Kijani

23. Zana ipi hutumika angani?
A. Bunduki
B. Nyambuzi
C. Mzinga
D. Jeti

24. Kanusha sentensi ifuatayo;
Mama anapika
A. Mama hapiki
B. Mama hajapika
C. Mama hatapika
D. Mama hupika

25. Kuumba ______ kunapendeza.
A. yote
B. kwote
C. kote
D. pote

26. ***Andika kwa wingi.***
Kalamu imepotea.
A. Kalamu haitapotea
B. Kalamu zitapotea
C. Kalamu zimepotea
D. Kalamu hazitapotea

27. Amevalia nguo nyeusi ___________
A. pepepe
B. fofofo
C. tititi
D. ndi

28. Akisami hii ni $^1/_6$
A. subui
B. sudusi
C. tusui
D. robo

29. Ukubwa wa neno nyumba ni
A. kinyumba
B. nyumba
C. jinyumba
D. jumba

30. Kiranja wetu ni ______________
A. safi
B. msafi
C. wasafi
D. mbora

**Soma habari hii kisha ujibu maswali 31 - 40.**

Wakenya wengi utawaona na vijiredio hasa nyakati za mikaragazano ya kombe la dunia au la Afrika ili kupata mwendelezo wa mechi hizo moja kwa moja. Muchuano ya mpira, biashara, tanzia, salamu na hadi yaliyojiri huchanganisha kwa kumzindua au kumpa habari za mambo leo.

Redio imechangia papana katika harakati za kukuza maendeleo, kuelimisha wananchi, kuhusu ugonjwa wa ukimwi, ukabila, ukeketaji wa akina dada, kupiga ufisadi, kuendeleza haki za watoto na hasa kuwapa vijana nafasi bora katika jamii.

Nchini kuna idhaa mbalimbali za redio mathalani, redio Jambo, KBC, redio Citizen na redio Maisha. Hakika redio hizi zinahitaji kupewa mkono wa tahania kwa kuweza kuchangia mno katika ukuzaji wa lugha na maendeleo.

Chombo hiki chafaa kupewa umuhimu hasa katika kuyatazama masuala nyeti yanayozikumba jamii zetu. Matatizo mengi hutuparamia kutokana na hali ya kutofahamishwa mambo mapya yatokeapo. Litakuwa jambo la busara ikiwa kila mmoja atasikiliza matangazo ili kuelemishwa.

---

31. Ni kweli kusema watu ______ hutumia redio
    A. wote
    B. wengi
    C. wachache
    D. jumla

32. Ni wakati upi ambao watu wengi hutumia redio?
    A. Jioni
    B. Asubuhi
    C. Michezo
    D. Siasa

33. Ni nini ambacho hakijatajwa katika makala haya ambayo hupatikana kwenye redio?
    A. Ukeketaji
    B. Ukabila
    C. Tanzia
    D. Ukimwi

34. Redio huchangia yafuatayo ila
    A. maendeleo
    B. kuelimisha
    C. kukana ukeketaji
    D. kuendeleza ugaidi

35. Vyombo vya habari husaidia vijana kivipi?
    A. Kuwafanyia kampeini
    B. Kuwatetea vijana
    C. Kuwapa nafasi bora katika jamii
    D. Kuwazuzuwa vijana

36. Kati ya redio zilizotajwa kwenye habari hii, ni ipi ndio idhaa ya taifa?
    A. Jambo
    B. Citizen
    C. Maisha
    D. KBC

37. Redio zinastahili ______________
    A. kushtumiwa
    B. mkono wa tahania
    C. kushushwa
    D. kusifiwa

38. Redio huchangia mno ukuaji wa
    A. ukulima
    B. lugha
    C. ukabila
    D. uzalendo

39. Redio hushughulikia masuala ___
    A. ukulima
    B. lugha
    C. ukabila
    D. uzalendo

40. Jambo lipi la busara ambalo mwandishi anatueleza
    A. kununua redio
    B. kupenda redio
    C. kusikiliza matangazo ya redio
    D. kusoma magazeti

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41 - 50.**

Sungura aliona kuwa amekuwa mkubwa. Akaenda mbali akirukaruka na kula nyasi. Jioni ikaingia, mara akakutana na Kala. "Naomba ewe sungura unifuate nyumbani kwangu. Mini nimekuandalia chakula kizuri sana ambacho hutakisahau utakapokula. Kila siku utakitamani chakula hicho. Kala alisema kwa upole, "Nashukuru sana kwa moyo wako wa ukarimu. Lakini wazazi wangu wamenilea malezi ya kutokuwa mchoyo. Sipendi kushiba na dada zangu watatu kushinda kwa njaa. Kwa nini na wao hatuwaaliki?" Sungura alishauri.

"Hilo si wazo baya hata kidogo. Inaonekana moyo wako ni mweupe pepepe kama ilivyo roho yako. Dada zako wako wapi?" Kala akauliza, "Si mbali na hapa? Nifuate na muda si muda tutafika. Utajionea mwenyewe furaha ya dada zangu kupata ualishi wako." Sungura alieleza.

Wakaandamana kikiri kala akichechemea kwa kuwa alikuwa kiguru. Wakaenda hadi wakafika nje ya pango. "Dada zangu wamelala fofofo. Mimi nitawaamsha huko ndani na wewe utulie hapa tuli." Sungura akasema kwa sauti ya ulaghai.

Sungura akajipenyeza pangoni. Kala hakuweza kustahimili kigugumizi. Sungura akajibu, "Dada zangu ni wagonjwa?"

**41.** Ni kweli kusema sungura ________

A. alikuwa mkubwa

B. ilikuwa kawaida yake kuondoka

C. ilikuwa mara kwanza sungura kuenda mbali

D. sungura alikuwa na watoto

**42.** Ni nini kilichomfanya sungura kuenda mbali?

A. Ilikuwa desturi yake

B. Alikuwa mjanja

C. Alikuwa mjinga

D. Alidhani ni mkubwa na tayari kwa yote

**43.** Sungura aliendelea kula nyasi hadi

A. asubuhi B. mchana

C. jioni D. adhuhuri

**44.** Sungura alikutana na nani?

A. Panya B. Kobe

C. Kala D. Punda

**45.** Kala alimsihi sungura waandamane naye kwa sababu amemuandalia nini?

A. Kitoweo B. Chakula

C. Maji D. Majani

**46.** Nani alisema hajalelewa kwa maisha ya uchoyo?

A. Kala B. Wote

C. Sungura D. Hakuna

**47.** Sungura alikuwa na "dada" wangapi?

A. Watatu B. Wawili

C. Mmoja D. Wanne

**48.** "Moyo mweupe pepepe" ni mbinu upi ya lugha?

A. Tasfida B. Nahau

C. Tanakali za sauti D. Methali

**49.** Makao ya Sungura ni wapi?

A. Kichakani B. Shimoni

C. Pangoni D. Nyumbani

**50.** Kati ya hawa wahusika ni yupi pumbavu?

A. Sungura B. Dada

C. Kala D. Hakuna